**OFISI YA UMOJA WA MATAIFA YA URATIBU WA MAMBO YA HISANI-OCHA-Katika Mstari.**
**Uchapishaji wa OCHA.**

## Kanuni ongozi kwa uhamisho wa ndani.

### Dibaji kwa kanuni ongozi na katibu mkuu wa mambo ya Hisani Bw. Sergio Viera de Mello.

Jamii ya hisani inazidi kujua upeo wa uhamisho wa ndani unaoathiri zaidi ya watu milioni 20 Duniani kote. Ilhali wajibu wa kulinda watu waliohamishwa kindani (WWK) uko kwanza kabisa katika serikali za mataifa na mamlaka ya mitaa, ni muhimu jamii ya kimataifa kuona jinsi bora inavyoweza kuchangia uongezaji kinga kwa WWK katika hali za mzozo na upeo. Tunalazimika pia kusanifu msaada wa hisani katika njia itakoyoendeleza ulinzi kwa WWK

Katika mfumo wa Umoja wa Mataifa, hatua kuu zimechukuliwa kuzidisha mwitiko unaofaa na wa wakati kwa mahitaji ya watu waliohamishwa kindani (WWK). Kamati inayosimama Kati ya Mawakala (KIKM) imenikabidhi wajibu wa kutenda kama ncha ya kuangalia katika mfumo wa UM (Umoja wa Mataifa) kwa mambo yanayohusiana na waliohamishwa kindani. Kwa kutimiza wajibu huu, nimejitolea nafsi kuzidisha ukubwa wa UM kwa jumla kuitika kwa hali za uhamisho wa ndani na pia kupandisha uratibu imara na mgawanyo dhahiri wa wajibu wa uasisi na uungaji mkono unaofaa kwa mawakala tendaji.

Katika muktadha huu, ninakaribisha toleo la kanuni ongozi kwa uhamisho wa ndani na mwakilishi rasmi wa katibu mkuu-kwa WWK: kanuni hizi, zinazo msingi katika sheria ya mataifa ya hisani iliyoko sasa, na vifaa vya haki za binadamu, zitafanya kama kipimo cha mataifa kuongoza serikali na hisani za mataifa na mawakala ya uendelezaji katika utoaji wa msaada na kinga kwa WWK.

KIKM yaunga mkono vikamilifu kanuni ongozi na imewatia moyo wanajumuiya wake kuzigawana na Bodi za utendaji na wafanya kazi wake, hasahasa wale walio uwanjani, ili

kuhakikisha kwamba kanuni zimetumiwa katika vitendo vyao kwa niaba ya watu waliohamishwa kindani.

Nina imani kwamba kanuni ongozi zaweza kucheza dhima kuu katika kupandisha utambuaji wa mahitaji ya WWK, kuhamasisha uungaji mkono miongoni mwa jamii ya hisani na kusaidia washiriki uwanjani kutafuta tatuzi wanapokabiliwa na mahitaji ya kinga na misaada ya waliohamishwa kindani. Kanuni pia zitasaidia serikali kutoa usalama na ustawi kwa watu waliohamishwa.

Ninatumai kwamba kila mmoja wenu atafanya iwezekanavyo kuhakikisha uenezaji mpana sana na utumiaji wa kanuni ongozi, ili kutimiza ustawi unaohitajika sana, katika hadhi na uchukuaji wa watu waliohamishwa kindani.

**Noti ya utangulizi**
**na mwakilishi wa katibu mkuu juu ya watu waliohamishwa kindani**
**Bw. Francis M. Deng.**

Jamii ya kimataifa imekabiliwa na kazi kubwa ya kuhakikisha kinga kwa watu waliong'olewa kwa nguvu kutoka kwenye nyumba zao kutokana na mizozo ya vurugu, kukiuka kwa hali ya juu kwa haki za binadamu na visa vingine vya kutisha. lakini ambao hubaki ndani mwa mipaka ya nchi zao zenyewe. Karibu daima, huteseka kwa ajili ya kukosa haki na matumizi maalum , dhiki na ubaguzi. Ni kukabiliana na kichocheo hiki kwamba kanuni ongozi kwa uhamisho wa ndani zilianzishwa.

Kanuni zatambua haki na dhamana zinazohusu kinga kwa waliohamishwa kindani katika awamu zote za uhamisho. Zinatoa kinga dhidi ya uhamisho kiholela, msingi kwa kinga na usaidizi mnamo wa uhamisho, na dhamana kwa kurudi salama, upataji makazi mapya na kujumuika na jamii tena. Ingawa hazifanyi kifaa cha kuunganisha, kanuni hizi zinaakisi na zinatokea pamoja na haki za binadamu za mataifa na sheria za ukimbizi.

Kanuni hizi zilianza kutayarishwa kwa muda wa miaka mingi ili kufuatilia udhamini niliopewa katika (mwaka wa) 1992 na Tume ya haki za binadamu na kuimarishwa na uamuzi uliofuata wa Tume na Mkutano wa wote. Mwanzoni niliulizwa kujifunza vyanzo na matokeo ya uhamisho kindani, hadhi ya waliohamishwa kindani katika sheria ya kimataifa, kiwango ambacho, mahitaji yao hushughulikiwa chini ya mipango ya uasasi wa sasa na njia za kustawisha kinga na usaidizi kwao.

Kwa upatanaji, ustawishaji, ulihitaji sheria na mifumo ya asasi kwa waliohamishwa kindani na misheni za nchi zinazohusika kushughulisha serikali na wengine katika maongezi kwa niaba yao Vimekuwa vitendo vikuu vya udhamini wangu. Katika ushirikiano na kikundi cha mabingwa wa sheria wa mataifa, nilitahini kiwango ambacho watu waliohamishwa kindani hupokea taarifa za matukio zinazofaa chini ya sheria ya mataifa na nilitoa "Mkusanyiko na uchambuzi wa kaida halali." (E/CN. 4/1996/52/Add 2) uchunguzi uligundua kwamba ilhali sheria iliyoko sasa ina toa taarifa za matukio thabiti kwa waliohamishwa kindani, kuna eneo kuu ambamo inashidwa kutoa msingi imara kwa kinga yao na usaidizi. Kisha, Tume na mkutano wa wote viliniomba kutayarisha mfumo sanifu unaofaa kwa waliohamishwa kindani. Hili lilisababisha uandikaji mswada wa kanuni ongozi ambazo zinataja tena kaida zilizoko na zinaomba ubainishaji wa eneo zisizo dhahiri na kujaza mapengo.

Baada ya kutoa kanuni ongozi kwa Tume katika 1998, Tume ilikubali azimio ikitambua kanuni ongozi na kusudi langu lililotajwa kama mwakilishi wa Katibu mkuu kuzitumia katika maongezi yangu yanayoendelea na serikali na hao wote ambao udhamini wao na vitendo vinahusiana na mahitaji ya waliohamishwa kindani. Tume pia ilitambua uamuzi wa Kamati inayosimama kati ya mawakala ambayo ilikuwa imekaribisha kanuni na kutia moyo wanajumuiya wake kuzigawana na bodi za utendaji zao na wafanyakazi, hasa uwanjani, na kuzitumia katika vitendo vyao kwa niaba ya waliohamishwa kindani.

Kanuni ongozi zapaswa kutoa uongozi wa thamani wa utendi kwa serikali, wenye mamlaka hodari, vyama vilivyo kati ya serikali na vyama visivyo vya serikali "NGOs" katika kazi zao na watu waliohamishwa kindani. Ni tumaini langu kwamba zitaenea kwa mapana na kupewa matumizi ya utendi uwanjani.

**Kanuni ongozi kwa uhamisho wa ndani.**

**Utangulizi: Eneo na kusudi.**

(1) Kanuni ongozi hizi zakusudia mahitaji dhahiri ya watu waliohamishwa kindani duniani kote. Zinatambua haki na dhamana zinazohusiana na kukinga watu wahamishwao kwa nguvu na kuwakinga na kuwasaidia wakati wa uhamisho wao pamoja na wakati wa kurudi kwao au upataji makazi mapya na kustareheka tena.

(2) Kwa makusudi ya kanuni hizi, watu waliohamishwa kindani, ni watu au vikundi vya watu ambao wamelazimishwa au wameshurutishwa kuacha au kukimbia nyumba au maskani yao, hasa kwa matokeo ya,au, ili kuzuia athari za mizozo ya silaha, hali za migogoro ya jumla, unyimwaji wa haki za binadamu au maafa ya kimaumbile au ya vitendo vya binadamu na ambao hawajavuka mpaka unaotambulika kimataifa wa nchi.

(3) Kanuni hizi huakisi na zinauthabiti na sheria ya haki za binadamu za mataifa na sheria ya mataifa ya hisani. Zinatoa mwongozo kwa:

(a) Mwakilishi wa Katibu mkuu wa watu waliohamishwa kindani katika utekelezaji udhamini wake;
(b) Mataifa yanapokabiliana na visa vya uhamisho wa ndani;
(c) Mamlaka mengine yote, vikundi na watu katika uhusiano wao na watu waliohamishwa kindani; na
(d) Vyama vya serikali na vile visivyo vya serikali vinaposhughulikia uhamisho wa ndani.

(4) Kanuni ongozi hizi zinapaswa kuenezwa na kutumiwa kwa mapana iwezekanavyo.

**Sehemu ya I: Kanuni za jumla.**

**Kanuni ya I**

1. Watu waliohamishwa kindani watafurahia vikamilifu haki sawa na Uhuru chini ya sheria ya kimataifa na ya nyumbani kama watu wengine wa nchi yao. Hawatabaguliwa katika ufurahiaji wa haki yoyote ile na uhuru kwasababu wamehamishwa kindani.

2. Kanuni hizi hazina athari kwa wajibu wa jinai wa mtu chini ya sheria ya kimataifa, hasa kuhusiana na uangamizaji, jinai dhidi ya ubinadamu na uhalifu wa vita.

**Kanuni ya 2**

1. Kanuni hizi zitatekelezwa na mamlaka yote, vikundi na watu bila kuzingatia hadhi zao za kisheria, na kutumiwa bila ubaguzi wa aina yoyote. Utekelezaji wa kanuni hizi hautaathiri hadhi ya kisheria ya mamlaka yoyote, vikundi au watu wanaohusika.

2. Kanuni hizi hazitafasiriwa kama za kuzuia, kugeuza au kudhalilisha uwekevu wa haki za binadamu za kimataifa zote zile, au vifaa vya sheria ya kimataifa ya hisani au haki zilizowapewa watu chini ya sheria za nyumbani. Kwa mahususi, kanuni hizi hazina athari kwa haki ya kutaka na kufurahia kimbilio katika nchi nyingine.

**Kanuni ya 3**

1. Mamlaka ya mataifa yana dhima ya msingi na wajibu wa kutoa kinga na usaidizi wa utu kwa watu waliohamishwa kindani katika mamlaka yao.

2. Watu waliohamishwa kindani wana haki ya kuomba na kupokea kinga na usaidizi wa kiutu kutoka mamlaka haya. Hawatateswa au kuadhibiwa kwa kufanya ombi hilo.

**Kanuni ya 4**

1. Kanuni hizi zitatumiwa bila ubaguzi wa aina yote, kama: Rangi, Kimaumbile, Lugha, Dini au Itikadi, Siasa au msimamo mwingine, Taifa au Kabila au Chimbuko la jamii, Sheria au Hadhi ya kijamii, Umri, Ulema, Ufukara, Kuzaliwa au vigezo vingine vyovyote kama hivi.

2. Watu wafuatao waliohamishwa kindani, kama vile watoto, hasa wadogo wasioandamanwa, wajawazito, akina mama wenye watoto wadogo, viongozi wa familia wa kike, watu wenye ulema, na wazee, watapewa haki ya kinga na usaidizi uhitajikao kwa hali yao na kwa kushughulikiwa kunakozingatia mahitaji yao rasmi.

**Sehemu ya II.  Kanuni zinazohusu kinga dhidi ya Uhamisho.**

**Kanuni ya 5**

Mamlaka yote na watendaji wa kimataifa wataheshimu na kuhakikisha heshima kwa masharti yao chini ya sheria ya kimataifa, mkiwemo haki za binadamu na sheria ya hisani, katika hali zote, ili kukinga na kuzuia hali zinazoweza kuleta uhamisho wa watu.

**Kanuni ya 6**

1. Kila mtu atakuwa na haki ya kukingwa dhidi ya kuhamishwa kiholela kutoka kwenye nyumba yake, mahali au maskani pa kuishi.

2. Mkatazo wa uhamisho wa kiholela ni pamoja na:

   (a) Unapokuwa na msingi juu ya sera za ubaguzi, “usafishaji wa kikabila” au vitendo kama hivyo vinavyolenga/ au vinavyotokea katika ugeuzaji kabila, dini au makini ya kimbari ya watu wanaohusika.
   (b) Katika hali za mizozo ya silaha, isipokuwa usalama wa raia wahusikao au sababu za lazima za kijeshi zinapodai.
   (c) Katika hali za miradi mikubwa ya kimaendeleo, ambayo hayathibitishwi kihalali na ulazimisho na upendeleo wa umma wenye puuzi;
   (d) Ikiwa ni maafa, ispokuwa usalama na afya vya wale walioathirika vinahitaji uhamishaji; na
   (e) Unapotumiwa kama adhabu ya wote.

3. Uhamisho hautaendelea kuzidi hali ya mambo inavyotaka.

**Kanuni ya 7**

1. Kabla ya uamuzi wowote ule uhitajio uhamisho wa watu, Mamlaka yanayohusika yatahakikisha kwamba chaguo badili zote ziwezekanazo zimejaribiwa ili kuepuka uhamisho kwa jumla. Pale ambapo hapana chaguo badili, vipimo vyote vitachukuliwa kupunguza uhamisho na athari zake mbaya .
2. Mamlaka yanayofanya uhamisho kama huo, yatahakikisha kwa kiwango cha utendi cha juu, kwamba, makazi mema yanapewa watu waliohamishwa, kwamba hamisho kama hizo zinatimizwa katika hali zinazoridhisha za usalama, Lishe, afya na usafi na kwamba wanajumuyia wa familia moja hawatenganishwi.
3. Uhamisho ukitokea katika hali zingine ispokuwa mnamo wa hatua za dharura za mizozo ya silaha na maafa, dhamana zifuatazo zitakusanywa na:

   (a) Uamuzi maalumu utachukuliwa na mamlaka ya taifa likiidhiniwa na sheria kuamuru hatua kama hizo.
   (b) Hatua zinazofaa zitachukuliwa kudhamini wale watakaohamishwa taarifa kamili juu ya sababu na taratibu za uhamisho wao na pale inapohitajika, kwa fidia na makao mapya.
   (c) Ukubalifu huria na unaojulikana kwa wale watakaohamishwa utatafutwa.
   (d) Mamlaka yanayohusika yatajitahidi kushughulisha wale walioathirika hasa wanawake, katika upangaji na uongozi wa makao mapya yao.
   (e) Hatua za kutia nguvu sheria pale zinapohitajika, zitachukuliwa na mamlaka halali yaliyo thabiti; na
   (f) Haki kwa tiba ya kufaa, mkiwemo kuangalia upya kwa uamuzi kama huo na mamlaka ya jaji yanayofaa, zitaheshimiwa.

**Kanuni ya 8**

Uhamishaji hautafanywa katika njia inayokiuka haki za uhai, hadhi, uhuru na usalama wa wale wanaoathirika.

**Kanuni ya 9**

Mataifa yako chini ya shurutisho mahususi kukinga dhidi ya kuhamisha watu wa asili, wachache, makabwela, wachungaji na vikundi vingine vinavyo utegemezi rasmi kwa kushikilia kwa ardhi zao.

**Sehemu ya III. Kanuni zihusuzo ulinzi mnamo wa uhamishwaji.**

**Kanuni ya 10**

1. Kila mwanadamu ana haki ya kurithiwa kwa uhai ambao utalindwa na sheria. Hakuna mmoja atakayenyimwa kiholela uhai wake. Watu waliohamishwa kindani watalindwa mahususi dhidi ya.
   (a) Uangamizwaji;
   (b) Mauaji;
   (c) Muhutasari au uuaji kiholela: na
   (d) Upoteaji wa lazima, mkiwemo utekwaji nyara au ufungwaji, usiojulikana, unaotisha au unaotokea katika kifo.

   Matishio na uchocheaji kutenda hayo yote vitakatazwa.
2. Mashambulio au vitendo vingine vya mgogoro dhidi ya watu waliohamishwa kindani ambao hawashiriki tena katika uhasama vimepigwa marufuku kwa hali yoyote. Watu waliohamishwa kindani watakingwa mahususi dhidi ya;
   (a) Mashambulizi waziwazi au yasiyotenganisha au vitendo vingine vya mgogoro, mkiwemo ubunifu wa maeneo ambayo mashambulizi kwa raia yanaruhusiwa.
   (b) Unyimwaji chakula kama njia ya mapambano.
   (c) Kutumiwa kukinga nia za kijeshi dhidi ya shambulizi au kukinga, kupendelea au kuzuia utendaji wa jeshi.
   (d) Mashambulizi dhidi ya kambi au makazi yao; na
   (e) Matumizi ya mabomu ya ardhi ya kua watu.

**Kanuni ya 11**

1. Kila mtu ana haki kwa heshima na uadilifu wa mwili, akili na tabia.
2. Watu waliohamishwa kindani, ama,au uhuru wao umezuiliwa, watalindwa mahususi dhidi ya:

(a) Ubakaji, kuatilika, mateso, ukatili, utendeaji usio wa kiutu au unaoshusha heshima au adhabu na vitendo viovu vingine juu ya uhuru wa mtu, kama vitendo vya migogoro ya kijinsia, ukahaba unaolazimishwa, na mtindo wowote wa shambulio la kuaibisha mtu hadharani,
(b) Utumwa au mtindo wowote wa kisasa wa utumwa, kama vile uuzwaji kwa ndoa, unyonywaji kingono au kazi ya kulazimisha kwa watoto; na
(c) Vitendo vya mgogoro vinavyolenga kueneza hofu miongoni mwa watu waliohamishwa kindani.

Matishio na uchocheaji kutenda hayo yote vitakatazwa.

**Kanuni ya 12**

1. Kila mwanadamu ana haki kwa uhuru na Usalama wa mtu. Hakuna mtu atakayekamatwa au kufungwa kiholela.
2. Kuipa uzito haki hii kwa watu waliohamishwa kindani, hawatafungiwa au kuwekewa mipaka katika kambi. Ikiwa katika hali ghairi, ufungiaji au uwekaji mipaka ni wa lazima, hautaendelea kuzidi inavyotakwa na hali hizo.
3. Watu waliohamishwa kindani watalindwa dhidi ya kukamatwa kunakotenganisha na kufungwa kama tokeo la uhamishaji wao.
4. Hakuna hali yoyote ambamo watu waliohamishwa kindani watachukuliwa mateka.

**Kanuni ya 13**

1. Hakuna hali yoyote ambamo watoto waliohamishwa wataajiriwa ama kutakwa au kuruhusiwa kushughulikia uhasama.
2. Watu waliohamishwa kindani watalindwa dhidi ya mazoea yanayotenganisha ya kuandikishwa katika vikosi vyenye silaha au vikundi, kama matokeo ya uhamishwaji wao. Kwa mahususi, ukatili wowote, mazoea ya kinyama au yanayoshusha hadhi, yanayoshurutisha ukubalifu au kuadhibu wasiokubali kwa uandikishaji vinapigwa marufuku kwa hali yoyote.

**Kanuni ya 14**

1. Kila mtu aliyehamishwa kindani ana haki ya uhuru wa kuhama na uhuru wa kuchagua maskani yake.
2. Kwa mahususi, watu waliohamishwa wana haki ya kuhama huria ndani na nje ya kambi au makazi mapya katika mahali popote ambapo uhai, usalama, uhuru, na/au afya vyao vingekuwa kwa hatari.

**Kanuni ya 16**

1. Watu wote waliohamishwa kindani wana haki ya kujua kilichowafikia au mahali walipo jamaa zao.
2. Mamlaka yanayohusika yatajibidiisha kutambua kilichowafikia na mahali walipo watu waliohamishwa kindani ambao wameripotiwa kuwa wamekosekana; na yatashirikiana na vyama vya mataifa vinavyoshughulikia kazi hii. Yatawaarifu ndugu za karibu zao juu ya maendeleo ya uchunguzi na kuwaarifu tokeo lolote lile.
3. Mamlaka yanayohusika yatajibidiisha kukusanya, na kutambua mabaki ya miili ya marehemu, yatazuia uoazaji na ushikaji mbaya, na yatawezesha kurudi kwa mabaki hayo kwa ndugu wa karibu au kuyazika kwa heshima.
4. Mahali pa kaburi pa watu waliohamishwa kindani palazimika kulindwa na kuheshimiwa kwa hali yoyote. Watu waliohamishwa kindani wanapaswa kuwa na haki ya kufika mahali pa kaburi pa marehemu jamaa zao.

**Kanuni ya 17**

1. Kila mwanadamu ana haki ya heshima kwa familia yake.
2. Kuipa uzito haki hii kwa watu waliohamishwa kindani, wanajumuyia wa familia ambao wanapenda kubaki pamoja, watakubaliwa kufanya hivyo.
3. Familia ambazo zimetenganishwa na uhamishaji ziunganishwe tena haraka iwezekanavyo. Hatua zote zifaazo zitachukuliwa kuharakisha uunganaji tena wa familia kama hizo, hasahasa kama watoto wamehusika. Mamlaka yanayohusika, yatarahisisha maulizo yanayofanywa na

wanajumuyia wa familia na kuwatia moyo na kushirikiana na kazi ya vyama vya hisani vinavyoshughulikia kazi ya kuunganisha familia tena.

4. Wanajumuyia wa familia zilizohamishwa kindani ambao uhuru wao umezuiliwa na kufungwa au kuwekewa mipaka katika kambi watakuwa na haki ya kubaki pamoja.

**Kanuni ya 18**

1. Watu wote waliohamishwa kindani wana haki kwa kiwango kifaacho ya kuishi.
2. Kwa kiwango cha chini, bila kujali hali, na bila kutenganisha, mamlaka yenye uhodari yatawapa watu waliohamishwa kindani na kuhakikisha ufikaji salama kwa:

   (a) Chakula kihitajikacho na maji yakuchukuliwa;
   (b) Mahali pa kujisetiri pa msingi na nyumba;
   (c) Mavazi yanayofaa; na
   (d) Matibabu yanayohitajika na usafi wa mazingira.

3. Jitihada rasmi zitapaswa kufanya kuhakikisha ushiriki kamili wa wanawake katika upangaji na usambazaji wa ugavi huu wa msingi.

**Kanuni ya 19**

1. Watu wote waliohamishwa kindani wenye majeraha au wagonjwa pamoja na wale wenye ulema watapokea kwa kiwango kikamilifu cha utendi na kwa kukawia kwa kiwango cha chini sana iwezekanavyo utibabu na utazamiwaji wanaotaka, bila utofautishaji juu ya nyanja zozote zile ispokuwa tiba. Ikitakikana, watu waliohamishwa kindani watapata ufikaji kwa huduma za kisaikolojia na za kijamii.
2. Uangalifu rasmi utawekwa kwa mahitaji ya kiafya ya wanawake, mkiwemo ufikaji kwa wakimu wa watunzaji afya wa kike na huduma, kama utunzaji wa afya ya uzazi pamoja na ushauri unaofaa kwa kafara wa kingono na matusi mengine.
3. Uangalifu rasmi pia utapewa uzuiaji wa magonjwa yakuambukiza na kuenea, mkiwemo UKIMWI miongoni mwa watu waliohamishwa kindani.

**Kanuni ya 20:**

1. Kila mwanadamu ana haki ya kutambuliwa popote kama mtu mbele ya sheria.
2. Kuipa uzito haki hii kwa watu waliohamishwa kindani, wenye mamlaka wanaohusika watawapa hati zote zihitajiwazo kufurahia na kuzoeza haki zao halali, kama vile, pasipoti, vyeti vyakumtambua mtu, vyeti vya kuzaliwa na vyeti vya ndoa. Kwa mahususi, wenye mamlaka watarahisisha upewaji wa vyeti vipya au kuviweka tena vile vilivyopotea mnamo wa uhamishaji, bila kuweka masharti yasiyo ya maana, kama vile, kuhitajika kurudi kwa eneo la maskani ya kawaida, ili kupata hivi au vyeti vingine.
3. Wanawake na wanaume watakuwa na haki sawa kupata hati kama hizi zinazohitajika na watakuwa na haki kupata hati kama hizi katika majina yao wenyewe.

**Kanuni ya 21**

1. Hakuna mtu atakayenyimwa kiholela mali na miliki.
2. Mali na miliki za watu waliohamishwa kindani zitalindwa kwa hali yoyote, kwa mahususi dhidi ya vitendo vifuatavyo:

   (a) Uporaji.
   (b) Mashambulizi ya moja kwa moja au yasiyotenganisha au vitendo vingine vya mgogoro.
   (c) Kutumiwa kukinga vitendo malengo ya jeshi.
   (d) Kufanywa kifaa cha kulipiza kasasi ; na
   (e) Kuharibiwa au kuchukuliwa kama aina ya adhabu ya jumla.

3. Mali na miliki zilizoachwa nyuma na watu waliohamishwa zitalindwa dhidi ya uharibifu na uchukuliwaji kiholela na usio halali, utumiwaji au umilikwaji.

**Kanuni ya 22**

1. Watu waliohamishwa kindani ama au wanaishi kambini hawatabaguliwa kama tokeo la uhamishwaji wao katika ufurahiaji haki zifuatazo.

(a) Haki za uhuru wa fikira, dhamiri, dini au itikadi, dhana na kujieleza.
(b) Haki ya kutafuta huria nafasi za kazi na kushughulika na vitendo vya kiuchumi.
(c) Haki ya kuungana na watu huria na kushiriki kwa usawa katika mambo ya jamii.
(d) Haki ya kupiga kura na kushiriki katika mambo ya kiserikali na ya Umma; mkiwemo haki yakufika njia zinazohitajika kutenda haki hii; na
(e) Haki ya kuwasiliana katika Lugha wanayofahamu.

**Kanuni ya 23**

1. Kila mwanadamu ana haki kwa Elimu.
2. Kuipa uzito haki hii kwa watu waliohamishwa kindani, wenye mamlaka wanaohusika watahakikisha kwamba watu kama hao, kwa mahususi watoto waliohamishwa, wapokee Elimu itakayokuwa huru na ya lazima kwa kiwango cha msingi. Elimu yapaswa kuheshimu utambuzi wao wa kitamaduni, Lugha na dini.
3. Jitihada rasmi ifanywe kuhakikisha ushiriki kamili na usawa wa wanawake na wasichana katika taratibu za Elimu.
4. Elimu na vifaa vya kufunzia vitapatikana kwa watu waliohamishwa kindani, hasa vijana na wanawake ama au sivyo wanaishi kambini, haraka hali zitakavyo kubali.

**Sehemu ya IV. Kanuni zinazohusiana na usaidizi wa hisani.**

**Kanuni ya 24**

1. Usaidizi wote wa hisani utatokea kulingana na kanuni za utu na zisizopendelea na bila ubaguzi.
2. Msaada wa hisani kwa watu waliohamishwa kindani hautachepuliwa, hasa kwa sababu za siasa au za kijeshi.

**Kanuni ya 25**

1. Dhima ya msingi na wajibu wa kutoa msaada wa hisani kwa watu waliohamishwa kindani viko mikononi mwa mamlaka ya kitaifa.
2. Vyama vya hisani vya kimataifa na Watendi wengine wafaao, wana haki ya kutoa huduma zao kuunga mkono waliohamishwa kindani. Toleo kama hili halitaangaliwa kama kitendo kisicho cha urafiki au mwingilio katika mambo ya ndani ya taifa, na litafikiriwa kwa moyo mwema. Ukubalifu kwahivyo hautazuiliwa kiholela, kwa mahususi wenye mamlaka wanaohusika wasipoweza au wasipotaka kutoa msaada wa hisani unaohitajika.
3. Wenye mamlaka wote wanaohusika watajalia na kurahisisha upitishaji huru wa msaada wa hisani na kuwajalia watu wanaoshughulika katika utoaji wa msaada kama huo ufikaji wa haraka na usiozuiliwa, kwa waliohamishwa kindani.

**Kanuni ya 26:**

Watu wanaoshughulika katika msaada wa hisani, usafiri wao na ugavi vitaheshimiwa na kulindwa. Hawatakuwa vifaa vya kushambulia au vitendo vingine vya mgogoro.

**Kanunui ya 27:**

1. Vyama vya kimataifa vya hisani na watendi wengine wafaao, wanapotoa msaada, hupaswa kuangalia mahitaji ya ulinzi na haki za binadamu vya watu waliohamishwa kindani na kuchukua hatua zinazofaa kuhusu suala hili. Kwa kufanya hivi, vyama hivi na watendi wapaswa kuheshimu viwango vya kimataifa vinavyohusika na kanuni za maadili mema.
2. Aya iliyotangulia haina dhuluma kwa wajibu wa ulinzi wa vyama vya kimataifa vilivyodhaminiwa kwa nia hii, ambavyo huduma zake zitapewa au kuombwa na mataifa.

**Sehemu ya V: Kanuni zinazohusu kurudi, kupata makazi mapya na kujumuika tena.**

**Kanuni ya 28**

1. Wenye mamlaka hodari wanadhima ya msingi na wajibu kuweka masharti pamoja na kutoa njia, zinazoruhusu watu waliohamishwa kindani, kurudi kwa hiari yao, katika usalama na heshima, kwa nyumba zao au maskani mwao, au kupata makazi mapya kwa hiari yao katika sehemu nyingine za nchi. Wenye mamlaka kama hao watajibidiisha kurahisisha ustarehekaji wa watu waliorudi au kupata makazi mapya, ambao walikuwa wamehamishwa kindani.
2. Jitihada rasmi zitawekwa kuhakikisha ushiriki kamili wa watu waliohamishwa kindani katika upangaji na uongozaji wa kurudi kwao na kujumuika tena..

**Kanuni ya 29**

1. Watu waliohamishwa kindani ambao wamerudi kwa nyumba zao au maskani yao au ambao wamepata makazi mapya katika sehemu nyingine za nchi, hawatabaguliwa kama tokeo la kuhamishwa kwao. Watakuwa na haki kushiriki vikamilifu na kwa usawa katika mambo ya umma kwa kiwango chochote na kupata ufikaji sawa kwa huduma za umma.
2. Wenye mamlaka hodari wana dhima na wajibu vya kuwasaidia waliorudi na/au waliopata makazi mapya ambao walikuwa wamehamishwa kindani, kupata tena, kwa kiasi kiwezekanacho, mali yao na miliki ambazo waliacha nyuma au walipokonywa walipo hamishwa. Upataji tena wa mali na miliki kama hizo usipowezekana, wenye mamlaka hodari watatoa au watasaidia watu hawa kupata fidia inayofaa au mtindo mwingine wa kupewa tena vitu walivyopoteza.

**Kanuni ya 30:**

Wenye mamlaka wote wanaohusika watajalia na kurahisisha kwa vyama vya kimataifa vya hisani na watendi wengine wanaofaa, katika utimizaji wa dhamana zao mfululizo, ufikaji wa haraka na usiozuiliwa kwa watu waliohamishwa kindani kusaidia katika kurudi kwao au upataji makazi mapya na kujumuika tena.